**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU- TAMISEMI**

SHULE YA SEKONDARI UMMY MWALIMU

S.L.P 6182

TANGA.

Tarehe:……………………

ummymwalimusecondary@gmail.com

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI UMMY MWALIMU WILAYA YA TANGA JIJI MKOA WA TANGA MWAKA WA MASOMO 2026.**

## 1.0 UTANGULIZI:

Ninafurahi kukuarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha tano katika Shule ya Sekondari Ummy Mwalimu mwaka wa masomo 2025/2026 na atasoma tahasusi ya PCM/EGM/HGL.

Shule ya Sekondari Ummy Mwalimu ipo kata ya Maweni, eneo la Saruji kilometa tano (5) kutoka kituo kikuu cha mabasi Kange. Kijiografia ni Eneo la kiwanda cha Saruji, karibu na shule ya msingi Saruji. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **06/07/2026** unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **04/07/2026**. Tarehe ya mwisho ya kuripoti shuleni ni …**/…./2026,** Kama hautaripoti shuleni hapa au umeamua kujiunga na shule binafsi au mashirika ya dini, mzazi/mlezi anatakiwa Kutoa taarifa ya maandishi ikieleza mahali au shule binafsi ambayo mtoto amejiunga kabla ya tarehe … /…/2026.

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

### 2.1 (A)SARE ZA SHULE

i) sketi mbili mshono wa rinda boksi kitambaa kizito cha suti ifike kwenye kifundo cha mguu - rangi ya damu Mzee (dark red)

ii) Nguo ya kazi (shamba dress) Mbili (2) rangi ya kijani ya ukwa mshono wa solo na juba la rangi ya

kijani ya ukwa kwa wanaovaa hijabu . M**wanafunzi haruhusiwi kuja na Nguo za nyumbani.**

iii) Sweta rangi ya damu ya Mzee linapatikana shuleni

iv) T-shirt ya rangi ya dark cream yenye nembo ya shule ya kuvaliwa jumatano na nje ya darasa inapatikana shuleni.

v) Mashati mawili meupe ya mikono mifupi

Vi) Nusu kanzu (rangi nyeupe) inayofika magotini.

vii) Hijabu (Juba) rangi nyeupe ya darasani

Viii) Viatu vyeusi vya darasani vyenye Kamba ambavyo havina kisigino kirefu (jozi mbili)

ix) Soksi nyeupe jozi mbili au zaidi

**NB**: Iwapo mzazi / Mlezi utashindwa kushona sare ya mwanafunzi kwasababu yoyote Ile, basi mwanafunzi anaweza kushona sare hizo kwa fundi wa Nguo anayepatikana shuleni kwa gharama zifuatazo:

i) Sketi mbili za rangi ya damu ya mzee - sh 46,000/=

ii) Nguo ya kazi (shamba dress) 2 rangi ya kijani ya ukwa - 60,000/=

iii) Mashati mawili meupe - sh. 20,000/=

iv) Sweta la shule rangi ya damu ya mzee - 16,000/=

v) T-shirt ya dark cream - 12,000/= (Inapatikana shuleni)

vi) kwa wanafunzi wanaovaa hijabu (sketi 1, Juba 1 na Nusu kanzu 1) 50,000. (Kwa mbili tsh 100,000/=)

vi) Kuweka muhuri au alama kwenye Nguo zote 5,000/=

Fedha hizo zilipwe kwa fundi wa kushona wakati mwanafunzi anaripoti shulenio.

B) Sare za michezo kwa shule hii ni kama ifuatavyo:

i) Tracksuit za dark blue Mbili (2)

ii) T-shirt za dark blue (2)

ii) Raba nyeupe jozi 1

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:**

i) Ndoo mbili (Lita 10) zenye mfuniko, sahani, kijiko na kikombe.

ii) Godoro dogo la futi mbili na nusu linapatikana shuleni kwa gharama 35,000/=

iii) Mwamvuli kwa ajili ya kipindi cha mvua.

iv) Shuka mbili za rangi ya pinki , Nguo ya kulalia (night dress) na Mahitaji mengine ya mtoto wa kike.

v) Taulo, malapa, mswaki, kanga/ vitenge viwili na yebo yebo nyeusi kwaajili ya nje.

Vi) Chandarua kimoja cha pembe nne.

vii) Madaftari makubwa yasiyopungua 14, kalamu za kutosha, mathematical set Moja na begi jeusi la mgongoni lisilo na maandishi.

viii) Sanduku imara la chuma (trunk) na kufuli kwaajili ya kuhifadhia vifaa vyake muhimu

ix) Ream mbili (2) A4 plain kwa mwaka aina ya Top kopie isiwe kampuni ya MONDI na rim mbili (2) za ruled.

x) Kwa wanaosoma somo la chemistry/ physics waje na Digital stop watch pamoja na scientific calculator (fx 99).

xi) Aje na kadi ya Bima ya Afya.

**2.3 Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| i | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| ii | Tahadhari | 5,000/= |
| iii | Nembo | 5,000/= |
| iv | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB**

Fedha hiyo yote ya Michango (i-iv) ilipwe kwenye akaunti ya shule namba 41710073197- SHULE YA SEKONDARI SARUJI kwenye tawi lolote la benki / wakala na mwanafunzi aje na risiti ya malipo ya benki ikiwa imeandikwa jina sahihi la mwanafunzi.

**2.4 Vifaa vya Usafi**

a) Tahasusi ya EGM walete ufagio wa Chelewa, Jembe lenye mpini, kwanja, hard broom na Toilet brush

b) Tahasusi ya PCM walete Ufagio wa chelewa, Jembe la mpini, kwanja, mopper na Ndoo yake.

c) Tahasusi ya HGL walete Ufagio wa chelewa, Jembe la mpini, kwanja, soft broom na Reki.

NB: Vifaa hivi vitapatikana shuleni.

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebisha kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo:

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii yote kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni jambo la lazima.
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalizi ya kujisomea **(Evening preparations).**

(d)Kuwahi katika wito **(Utii wa kengele)** na kutekeleza kwa ufanisi shughuli zote za shule

(e) Kufahamu mipaka ya shule kwa kikamilifu, maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule. Usafi wa mwili na mavazi ni muhimu kuzingatia. Aidha ukaguzi utafanywa mara kwa mara kuweka msisitizo wa usafi na mavazi kwa usahihi.
(g) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(i) Kutunza mali za Umma.
(j) Ni marufuku kwa mwanafunzi kuja na simu ya mkononi, redio, headphones, earphones,Baruti, CD, Flash au kifaa chochote cha kielektroniki shuleni. Aidha simu au chombo chochote cha kielektroniki atakachokamatwa nacho mwanafunzi kitateketezwa na hakitarudishwa kwa mzazi wala mtoto, Usijisumbue kudai. Adhabu kali itatolewa kwa mwanafunzi husika.
(k) Lugha ya mawasiliano hapa shuleni ni kiingereza.
(l) Mwanafunzi atakapofika shuleni awe amekata nywele robo inchi na zisiwe na dawa. Shule hairuhusu kusuka nywele.

**MUHIMU:**

- Mwanafunzi haruhusiwi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.
- Mwanafunzi anapokuwa shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa.
- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. ( Msiba au Ugonjwa).
- Kutakuwa na "visiting day" kwaajili ya kumtembelea mwanafunzi wakati wa mahafali ya "O" level na "A" level. Taarifa itatolewa kwa wanafunzi.
- Kutakuwa na kikao cha wazazi kila jumamosi ya mwisho ya mwezi Machi. Kila mzazi anatakiwa kuhudhuria kikao hiki.

### 3.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE.

(a) Wizi na Ukabaji

(b) Ubakaji, ulawiti, usagaji na mahusiano yote ya kimapenzi kwa ujumla.

(c) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa Bangi, shisha, Cocaine, Mirungi, Kuberi na Ugoro pamoja na sigara.

d) kutembea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.

e) Kushiriki matendo ya uhalifu na matendo yoyote yale yanayovunja Sheria za nchi.

f) Kuolewa.

g) Kupata mimba, kutoa mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule.

(d) Kupigana au Kupiga (ndani na nje ya shule).

(e) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.

(f) Kudharau Bendera ya Taifa.

(g) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

(h) Kukataa adhabu kwa makusudi.

(i) Kuwa na simu ya mkononi, redio na pasi ya umeme au kifaa chochote kinachotumia umeme.

j) kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k

**3.3 KANUNI NA SHERIA ZA ZIADA ZA SHULE YA UMMY MWALIMU SEKONDARI.**

1. Ni marufuku mwanafunzi kusinzia darasani.
2. Ni marufuku kwa mwanafunzi kufuga nywele, kucha, kupaka piko, hina, rangi, kunyoa upara, viduku, kujichubua (skin bleaching).
3. Ni marufuku kutoka nje ya eneo la shule bila ruhusa.
4. Ni marufuku kuandika ukutani au kwenye samani za shule. Ukibainika utaleta ndoo ya rangi ya lita 20, brush ya kupakia rangi na kulipa gharama ya ufundi wa kupakia rangi.
5. Ni marufuku kula darasani na kutupa takataka ovyo ndani na nje ya madarasa
6. Ni marufuku kuwa na begi lenye maandishi ya hovyohovyo
7. Kila mwanafunzi anatakiwa kutunza mazingira wakati wote.
8. Kwa wasichana kutia dawa, kubana nywele hairuhusiwi , kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na nywele fupi zilizo nyolewa sawa kichwa kizima.
9. Ni marufuku kuja na vifaa au nguo zisizotakiwa shuleni mfano bangili, hereni,mikufu n.k.
10. Ni kosa kufanya udanganyifu kwenye mitihani
11. Au endapo mwanafunzi atakimbia kufanya mtihani wowote hapa shuleni hatua kali za nidhamu zitachukuliwa dhidi yake , ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo

**4:0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

a. Medical Examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti( Appendix D)
b. Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi (A) na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai (kiambatanisho B)
c. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria ,kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule (kiambatanisho C)
d. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
e. Nakala ya cheti cha matokeo kidato cha nne (Result slip)

**5:0 MITIHANI**

Kila muhula wanafunzi wanafanya mitihani na matokeo kutumwa kwa wazazi/walezi. Mtoto wako ajitahidi asipate wastani wa alama za chini ya 50%. Shule pia inatoa majaribio ya ziada kwa kushirikiana na kamati ya wazazi, kwa mwezi wanafanya mitihani ya masomo yote na matokeo yanabandikwa shuleni wiki moja baada ya mitihani kufanyika. Ikiwa mzazi/mlezi hupati matokeo ya mitihani ya mwanao ya kila muhula na yale ya kila wiki, wasiliana na shule haraka iwezekanavyo.

**6:0. MUHIMU SANA**

- Tafadhali soma kwa makini **masharti** ya shule hii. Mwanafunzi anayejiunga Ummy Mwalimu sekondari hategemewi kuvunja sheria/kanuni na taratibu za shule kwani akifanya hivyo ni kwa makusudi na siyo bahati mbaya na hatua za kinidhamu zitachukuliwa mara moja.
- Utakaporudisha fomu hii ,mzazi tunaomba urudishe ndani ya faili la plastiki la rangi nyekundu (spring file). Mafaili yanapatikana shuleni.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

……………………………………….

ASHA . S. KITUNDU

**MKUU WA SHULE**

**NB:**

Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mtandao) . Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi na kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi, hivyo mzazi atume pesa.

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/ MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:**

- Mkuu wa Shule - 0713628863/ 0789947894
- Makamu Mkuu wa Shule - 0786088101
- Mwalimu msaidizi wa malezi - 0788284161

**KIAMBATANISHO A**

**SHULE YA SEKONDARI UMMY MWALIMU**

**HISTORIA YA MWANAFUNZI**

Sehemu hii ijazwe na mwanafunzi

1.Jina kamili la mwanafunzi(kama lilivyotumika kwenye PREM)……………………………….

2.a. Tarehe ya kuzaliwa ..........................................

b.Sehemu alipozaliwa kijiji/ mtaa……………………………………....................................

Kata……………………… Wilaya………………………………Mkoa…………………….

3.Dini/dhehebu………………………………………………………………………………

4. Uraia……………………………………………………………………………………

5.a. Shule ya Sekondari aliyomaliza Kidato cha nne……………………………………………

b. Anuani ya shule ya Sekondari aliyomaliza kidato cha nne………………………..

c. Shule aliyotoka (kwa wahamiaji)……………………………………………………..

d.Shule zingine alizo soma kabla ya kuja UMMY Mwalimu sekondari ( kwa wahamiaji)

,.................................................

6.Afya (taja magonjwa yote makubwa uliowahi kuugu mfano TB, Polio, kifafa, pumu nk……………...

7.a. Jina la mzazi

i.mama…………………………………………………..(hai/amefariki)…………………………..

ii.Baba…………………………………………………..(hai/amefariki)…………………………..

b.Kazi ya mzazi/mlezi

i.Baba……………………………………………………………………………………………….

ii.Mama……………………………………………………………………………………………….

Anuani ya mzazi/ mlezi………………………………………………………………..

Namba ya simu ya baba………………………………… na mama……………………...

8.a.Jina la atakaye gharamia mahitaji yake ya shule……………………………………………

b. Anuani yake ni ……………………………………………………………………………….

c. Namba yake ya simu ……………………………Uhusiano………………………………kama kaka, dada, mjomba nk.

**UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI (SEHEMU HII IJAZWE NA MZAZI/MLEZI)**

**KIAMBATANISHO B**

**SHULE YA SEKONDARI UMMY MWALIMU**

| MZAZI/MLEZI WA KIKE | MZAZI/ WA KIUME |
|---|---|

Mimi ……………………………………………………………………………, mzazi/Mlezi wa mwanafunzi .................................................................. ninakiri kuzisoma na kuzielewa taratibu/sheria za shule ya sekondari Ummy Mwalimu, hivyo nakubali mwanangu ajiunge na shule ya sekondari Ummy mwalimu na nitamtimizia mahitaji yote ya shule kwa jinsi ilivyoagizwa. Pia naahidi kushirikiana na shule kumlea kitabia na kimaadili.

Saini ya mzazi/mlezi…………………………………………… Tarehe .............................................

**KIAMBATANISHO C**

**SHULE YA SEKONDARI UMMY MWALIMU**

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi ……………………………………………………………………….. nakubali kuchukuwa nafasi niliyopewa kujiunga na kidato cha tano mwaka 2026 katika Shule ya Sekondari Ummy mwalimu. Ninaahidi kufuata sheria na masharti yote . Na kwamba nitakapo toka shule wakati wa likizo nitarudi moja kwa moja nyumbani bila kupitia sehemu yeyote. Pia nitafikisha kwa wazazi barua ,maagizo na matokeo ya mitihani. Mwisho naahidi kujisomea kwa bidii, kushirikiana na wenzangu katika shughuli za masomo, kazi za nje, michezo na kufanya vizuri katika mitihani yangu na kupata wastani wa daraja A hadi C kwa kila somo.

……………………………………… ……………………………………….

**SAHIHI YA MWANAFUNZI** **TAREHE**

**APPENDIX D**

**UMMY MWALIMU SECONDARY SCHOOL**

**Box 6182**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

STUDENTS NAME………………………………………………………………………………

PART A (To be completed by Government medical Officer)

To medical officer

…………………………………………………………………………………………………….

…………………………………………………………………………………………………….

Please examine the above named student as to his/her fitness for admission as a student in this school.

Eyes……………………………………………………………………………………………..

Hearing………………………………………………………………………………………

Speech………………………………………………………………………………………….

Leprosy………………………………………………………………………………………….

Epilepsy………………………………………………………………………………………..

Venereal disease……………………………………………………………………………….

Neuroses………………………………………………………………………………………

Chest……………………………………………………………………………………………..

Abdomen………………………………………………………………………………………

Heart problem…………………………………………………………………………………

Blood pressure…………………………………………………………………………………..

Pregnancy (for females)……………………………………………………………………….

Others…………………………………………………………………………………………….

PART B (TO BE COMPLETED BY GOVERNMENT MEDICAL OFFICER)

I have examined the above and consider that……………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

………………………………………. SIGNATURE …………………………………….DATE

STATION………………………….. DESIGNATION……………………..